



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA



TANGAZO LA KUENZA KUPOKEA MAOMBI YA LESENI KWA KAMPUNI ZA UKUSANYAJI NA UGAWAJI WA MIRABAHA (COLLECTIVE MANAGEMENT ORGANIZATIONS – CMOs) TANZANIA BARA.

Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999 kama ilivyofanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Fedha Na. 1 ya mwaka 2022 na kuruhusu uanzishwaji wa Makampuni binafsi yatakayokuwa na jukumu la kukusanya na kugawa Mirabaha kwa pamoja yaani *Collective Management Organizations* (CMOs).

Kampuni yoyote yenye nia ya kupatiwa Leseni ili kufanya kazi kama CMOs Tanzania Bara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 inakaribishwa kuwasilisha maombi rasmi COSOTA kwa kuzingatia vigezo vinavyopatikana katika Kanuni za Hakimiliki na Hakishiriki (Kampuni za Ukusanyaji na Ugawaji wa Mirabaha), 2023, Toleo Namba 215 na 211 la tarehe 24 Machi, 2023. Kanuni hizi pia zinapatikana katika tovuti ya Ofisi: www.cosota.go.tz

Masharti ya kupatiwa leseni kwa kampuni ni kama ifuatavyo;

1. Iwe inamilikiwa na watanzania
2. Nakala ya picha za wamiliki (passport size)
3. Iwe na Hati ya namba ya mlipakodi (TIN) kutoka Mamlaka ya mapato Tanzania
4. Iwe na hati ya mlipa kodi (Tax clearance certificate) kutoka Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA)
5. Iwe na Leseni ya biashara kutoka mamlaka husika
6. Iwe na cheti ya usajili wa jina la kampuni kutoka BRELA
7. Iwe na hati ya usajili wa makampuni (Certificate of incorporation)
8. Iwe na Memorandum and Article of Association
9. Iwe na wasifu wa wamiliki
10. Iwe na taarifa za kibenki kwa kipindi cha miezi kumi na mbili
11. Iwe na uwezo wa kukusanya na kugawa mirabaha kwa ufanisi.
12. Iwe na Wanachama wasiopungua thelathini ambao inatarajia kuwawakilisha
13. Iwe haijawahi kupatikana na hatia ya ukwepaji kodi au uhujumu uchumi
14. Kufuata sheria na kanuni zote za Nchi;

Tafadhali tambua kuwa: Maombi ya Leseni yatapokelewa ndani ya siku 14 kuanzia tarehe 03 Mei, 2023, ya tangazo hili na yawasilishwe kupitia anuani ifuatayo:

Katibu,
Bodi ya Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA),
S.L. P 6388,

Dar es Salaam.

Tafadhali andika neno “CMO” juu ya bahasha.

Imetolewa na;
Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA),
S.L.P 6388, **Dar es salaam.**
SIMU: 0738 015 013

